MWONGOZO WA JAMII NA WAATHIRIKA WENGINE

1. Ofisi ya Uwajibikaji (OA) ni nini na inawezaje kuisaida jamii yangu?

OA inatatua wasiwasi na migogoro ya kimazingira au kijamii inayotokea katika miradi inayopata usaidizi wa OPIC, ikiwa ni pamoja na athari kwa mazingira, haki za binadamu, haki za kitamaduni na masuala ya haki za leba. OA inatoa jukwaa kwa washika dau walioathirika (k.m. jamii za karibu na wafanyakazi wa mradi) la kuibua wasiwasi kama hizo na la kujaribu kuzitatua.

2. OA inatoa huduma za aina gani?

OA inatoa huduma mbili: kutatua matatizo na pitio la uambatanaji.

3. Ninaweza kutarajia nini kutoka kwa huduma hizi?

Kwa mbinu ya kutatua matatizo, OA itajaribu kuunda hali zinazofaa kwa jamii zilizoathirika na mteja wa OPIC ili kutatua mgogoro kwa namna inayokubalika kwa pande zote mbili. OA haichukui msimamo kwa madai yoyote yanayoweza kuhusiana na mgogoro.

Kwa mchakato wa pitio la uambatanaji, OA itachunguza na kuripoti kuhusu utekelezaji wa OPIC wa sera husika. Ripoti hii inaweza kujumuisha mapendekezo ya jinsi OPIC inavyoweza kuimarisha matumizi yake ya sera katika mradi husika au katika miradi ya siku zijazo.

4. Nitajuaje kama huduma ya kutatua matatizo au ya pitio la uambatanaji ndiyo inayonifaa?

Maombi ya huduma yanaweza kufanywa ya kutatua matatizo au pitio la uambatanaji, zote mbili pamoja, na kwa mpangilio wowote. Ikiwa hauna uhakika ni huduma gani kati ya hizi mbili inakufaa, sio lazima ubainishe katika ombi lako, na unaweza kuwasiliana na Mkurugenzi wa Uwajibikaji kupata mwongozo.

5. Ninahitaji kujumuisha taarifa zipi katika ombi langu?

Maombi yanafaa kujumuisha taarifa zifuatazo:

- Utambulisho wa mtuma ombi na taarifa zake za mawasiliano.
- Utambulisho, taarifa za mawasiliano na stakabadhi za mwakilishi yeyote wa mtuma ombi, na ushahidi wa mamlaka ya mwakilishi kumwakilisha mtuma ombi.
- Kama mtuma ombi angependa utambulisho wake na/au taarifa zake zilizotolewa kwa Ofisi ya Uwajibikaji ziwekwe faraghani, na kutoa sababu.
- Aina na eneo la mradi ambao ndiyo mada ya ombi hilo, utambulisho wa mfadhili wa mradi (ikiwa anajulikana), na kama mradi huo kwa sasa unapata usaidizi wa OPIC (ikiwa inajulikana).
- Kauli ya madhara au hatari za athari mbaya za kimazingira, kijamii, haki za wafanyakazi au haki za binadamu zinazohusiana na mradi huo.
- Taarifa zozote za ziada zinazodhaniwa kuwa muhimu na mtuma ombi.

6. Ninaomba huduma vipi?

Una chaguo kadhaa za kuwasilisha ombi kwa maandishi, kulingana na namna inayokufaa zaidi. Ombi lako linaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza au kwa lugha yako ya asili.

- Unaweza kutuma barua pepe kwa accountability@opic.gov ukijumuisha taarifa zilizo hapa juu katika mwili wa barua pepe.
- Unaweza kujaza fomu inayofuata (Fomu ya Maombi ya Waathirika au Wawakilishi Wao) na uitume kama ambatisho kwenye barua pepe kwa accountability@opic.gov.
- Unaweza kutuma barua iliyo na maelezo yaliyo hapa juu kupitia barua pepe, faksi, au kuwasilisha kwa mkono.

Taarifa za mawasiliano za OA ni kama ifuatavyo:

Director, Office of Accountability
Overseas Private Investment Corporation
1100 New York Avenue, NW
Washington, DC 20527 USA

Simu 1-202-357-3910
Faksi 1-202-408-5133

Barua pepe: accountability@opic.gov

7. OA itaamuaje kama ombi langu linafaa?

OA itatathmini ombi lako kulingana na vigezo vifuatavyo:

- Ikiwa watuma maombi wanastahiki (mtu yeyote binafsi, kundi, jamii au mhusika mwingine walioathiriwa au wanaoweza kuathiriwa na mradi unapata usaidizi wa OPIC, au mfanyakazi katika mradi unaopata usaidizi wa OPIC)
- Ikiwa wawakilishi wowote wa watuma maombi wanawatambulisha watu wanaowawakilisha kwa uwazi, na ushahidi wazi wa mamlaka ya uwakilishi kutolewa kwa OPIC;
- Kama OPIC kwa sasa ina uhusiano amilifu wa kifedha na mradi;
- Ikiwa ombi lina madai ya athari au hatari kubwa, za moja kwa moja na mbaya; na
- Ikiwa kuna uhusiano mzuri kati ya mradi na athari zinazodaiwa.

8. Ni nini kinatendekea ombi baada ya kuwasilishwa?

OA itakuarifu kwamba imepokea ombi lako, na kukuarifu kama ombi lako linastahiki au la. Ikiwa ombi lako linastahiki, OA itatembelea eneo la kazi ili kuamua hatua mwafaka za kufuatwa. Ikiwa ombi lako halistahiki, OA itakuarifu, na kukupatia sababu ya ombi lako kutostahiki, na kupendekeza njia zingine wasiwasi zako zinaweza kutatuliwa. Kwa mfano, mbinu za migogoro zimewekewa baadhi ya miradi ya OPIC.

9. OA itashughulikiaje taarifa za faragha?

Kwa ujumla, OA inajaribu kuwa wazi katika huduma zake. Ombi likitumwa moja kwa moja, OA itadumisha faragha ya utambulisho wa watuma maombi wanaotaka hivyo, taarifa za wamiliki wa biashara, na taarifa nyingine zisizo za umma. OA haikubali maombi ya huduma bila jina.

10. Ni hali gani ambazo hazijumuishwi katika huduma za OA?

OA haikubali maombi kutoka kwa watuma maombi wasiostahiki, au yasiyo na kiwango cha chini zaidi kinachohitajika cha taarifa. OA haishughulikii masuala kuhusu ufisadi au shughuli nyingine za kijinai, masuala ya kibiashara/kimkataba, au utoshelevu wa sera za OPIC ili kuzuia madhara.